

Mnyeti awatangazia neema wauza samaki

Na **Elizabeth Seleman**, SENEREMA

NAIBU Waziri wa Mifungo na Uvuvi, Alexander Mnyeti, amewaondoa hofu wafanyabiashara wa Soko Kuu la Samaki la Migombani lililopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema kuwa, liko mbioni kufanyiwa ukarabati ili biashara kufanyika katika mazingira rafiki.

Mnyeti alitoa kauli hiyo juzi katika mukutano mkuu wa kupokea taarifa ya utekelezaji miradi Jimbo la Sengerema ambapo alisema, serikali inatarajia kuanza utaratibu wa kukarabati soko hilo.

Alisema soko hilo ndilo linalosambaza samaki Kanda ya Ziwa hivyo lazima ku-hakikisha miundombinu yake imekaa katika hali ya kuridhisha.

Pia alisema serikali itahakikisha inafanya ukarabati wa mabwawa ya Sengerema na kufufua mialo yote ambayo kwa sasa haitumiki kwa sababu ya kukosa miundombinu. Mnyeti aliwataka wavuvi kucha uvuvi haramu badala yake watumie boti ambazo zinatolewa na serikali ili kusaidia kuondoa usumbufo wa kuingia ziwani na kuvua bila kuwa na uhakika wa kupata samaki.

Mbunge wa Sengerema, Tabasamu Mwangao, aliiomba serikali ikamilishe miradi ambayo imeanzishwa ikiwamo ya elimu iliyoanzishwa na kusubiri ukamilishwaji. Kuhusu soko hilo, Tabasamu alisema endapo litafanyiwa maboresho vijana wanatachangamkia fursa ya kusambaza samaki na kujiinua kiuchumi.